

Nafasi Ya Pili

Roho wa Mungu aliutabiri wakati ambao walimu wa uongo watatokea, wakifundisha kila aina ya mafundisho ya uongo, 1 Timotheo 4:1-3. Moja ya mafundisho potofu ya hivi karibuni yaliyolumiza kanisa ni yale kwamba wakristo wanatakiwa kuishi maisha ya bila dhambi na endapo wangetenda dhambi, haibaki dhabihu kwa ajili ya dhambi zao.

Mtu mmoja kwa jina Herme, aliyekuwa mtumwa hapo awali, na ndugu yake na Pius mzee wa kanisa kule Rumi. Mnamo mwaka 150 aliandika jarida lililojulikana kama mchungaji wa Herme. Aliandika kitabu ili kukosoa dhana potofu ya kwamba hakuna msamaha wa dhambi kwa mkristo anayetubu.

Unachukuliaje kuishi maisha ya bila nafasi ya pili? Yangakuwa ya papo kwa papo. Tunahitaji nafasi ya pili. Kila nafsi iliyo hai, inayopumua itahitaji nafasi ya pili, tatu, nne au nafsi ya “pili” zaidi.

Ni mahali gani tunapohitaji nafasi ya Pili?

1. Kuna wale ambao wamewakosea watu wa familia fulani. Bila nafasi ya pili, pande zote zaweza kufa huku wakiwa na kinyongo.
2. Katika ndoa, kwa kiasi kikubwa haiwezekani kuishi na mtu fulani maisha yako yote bila kuumiza hisia za mwenza wako. Bila nafasi ya pili, kila ndoa ingeishia na talaka.
3. Katika utafutaji wa ajira makosa yatatokea. Bila kuwepo fura ya kujifunza kutokana na makosa, tusingefaa au kuwa waajiriwa bora.
4. Umewahi kuendesha gari? Ni hakika utafanya makosa. Askari wa barabarani anasogelea dirishani kwako, unadhani si vyema kujua kuwa kuna wakati anatoa nafasi ya pili?
5. Umewahi kucheza mechini nzuri ya mpira laini? Kwa kawaida tulikuwa tunakuwa na waya wa umeme umening’inizwa kwenye uwanja wetu, mpira ukigonga waya, mchezaji anakuwa ametoka nje. Kwa hiyo kwa haraka tulikuja na kanuni ya “rudia tena”
6. Halafu kuna maisha. Hii ndiyo jumla ya maneno; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Mhubiri 12:13. Na bado ukiwa kama mimi, mimi nimeshindwa daraja fulani. Siyo tu kabla sijaongoka, bali baada, na kwa hiyo nina hatia ya makosa, 1Yohana 3:4. Ingawaje makosa yangu hayatokuwa makubwa sana katika macho ya

watu, mbele za Mungu nimeanguka na kupungukiwa na utukufu wa wake, na ujira wangu kwa hakika ni mauti, Warumi 6:23

Namhimidi Mungu kwa nafasi ya pili, tatu, nne, tano.... Si ndiyo maudhui ya hadithi ya mwana mpotevu? Alienenda kwa namna ambayo siyo tu ilimpelekea kutenda dhambi, bali kumpa Mungu kisogo. Kijana aliangukia katika lindi la upweke. Na mara alipozingatia moyoni, alijinyenyekeza kwa Babaye, akiomba tu chakula na pa kulala. Lakini, hivi unafahamu yule Baba alifanyaje? Hakumpa tu chakula na pesa kidogo na kumfukuza. Hakumrudisha nyumbani kwa shingo upande. Alimrejeza mwanawe. Alirudishiwa nguo zake, chumba cha kulala, na madaraka. Baba alizidisha huruma na bila karipio wala adhabu, akampa nafasi ya pili, Luka 15:11-32.

Si tu tunahitaji nafasi ya pili, bali tukiwa katika Kristo, tunazizidisha. Si tu kwa sababu kuna hili tishio kutoka kwa Yesu kwamba endapo tunashindwa kutoa nafasi ya pili, “msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu” Mathayo 6:14. Bali, tutasamehe kwa sababu ya kuwa kama-Kristo, hutufundisha kwamba kusamehe na kutoa nafasi ya pili ni tabia ya ki-Mungu.